



## EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

# TANGAZO LA ZABUNI YA KUTOA HUDUMA ZA URATIBU KWENYE EACOP NCHINI TANZANIA NA UGANDA - NAMBA YA KUMBUKUMBU: 10004943

Total east Africa Midstream B.V (TEAM) inawakaribisha makandarasi wenye uzoefu na sifa ambao wameonyesha uwezo, nia na ambao wako tayari kutoa huduma za uratibu wa ndani na wa kimataifa kama ifuatavyo:

- Usafiri wa ndani na wa kimataifa kutoka ofisi za FCA hadi kwenye eneo la kazi nchini Uganda na Tanzania kwa kutumia mtoa huduma wa kitaifa
- Vibali vyote vya (kusafirisha nje na kuingiza ndani ya nchi, vya muda na vya kudumu)
- Mfumo uliunganishwa kwa kutumia mtandao (wa ndani na kimataifa) kwa mizigo na vyombo vya usafiri, ndege na malori
- Usimamizi wa bohari za muda
- Shughuli za upangaji wa mizigo

### Maelezo ya jumla

Mradi wa EACOP unajumuisha uhandisi, ujenzi, uendeshaji na matengenezo ya bomba la mafuta lililolofukiwa chini ya ardhini Tanzania na Uganda likiwa na mfumo wa umeme wa kuleta joto pamoja na miundombinu iliyo juu ya ardhini na kituo cha kuhifadhi mafuta cha baharini kilichopo Chongoleani, karibu na bandari ya Tanga

### Sifa za msingi:

- Kuwa na ofisi kwenye maeneo yote husika

(Marekani-Asia-Ulaya-Mashariki ya Kati -Tanzania -Uganda

- Uzoefu kwenye sera, taratibu na mchakato wa afya, usalama, mazingira, jamii na ubora ili kuendana na Viwango vya Utendaji vya IFC na viwango vya kimataifa vya sekta husika
- Uzoefu wa miaka 10 kwenye shughuli za usambazaji wa mizigo, uzoefu kwenye usimamizi wa bohari na wauzaji kwenye miundo mbinu ya mafuta na gesi barani Afrika na duniani kote
- Kuwa na wafanyakazi wenye vyeti na uzoefu kwa ajili ya kufanya kazi kwenye mradi
- Kuwa na vifaa stahiki vinavyoendana na viwango vya sekta husika na vilivyothibitishwa
- Kuwa na uwezo wa kifedha kwa ajili ya kutoa huduma
- Kuheshimu sheria na kanuni za serikali za Tanzania na Uganda  
(TZ: Sheria ya Mafuta (kifungu cha 392) ya mwaka 2017  
(UG: Sheria ya Mafuta ya mwaka 2013 na hati za kisheria za mwaka 2016 namba 34) ikiwa ni pamoja na usajili kwenye Kanzi data ya Taifa ya watoa huduma (NSD) inayotunzwa na Mamlaka ya Mafuta ya Uganda (PAU) kwa ajili ya watoa huduma kwenye sekta ya mafuta na gesi
- Uzoefu kwenye usimamizi wa HLOOG (mitambo mikubwa) ya usafirishaji

Makampuni yenye sifa za msingi na yenye uwezo wa kutoa huduma zilizotajwa hapo juu, yaombe fomu ya zabuni kwa kutuma barua pepe kwa: [ep.eacop-log-eoi-lsp@total.com](mailto:ep.eacop-log-eoi-lsp@total.com) kabla ya Ijumaa tarehe **9 Februari 2018, saa 6.00 mchana kwa saa za Kampala.**

Utoaji wa fomu ya maombi ya zabuni kwa makampuni husika utaendana na kusainiwa kwa Makubaliano ya Kutunza Siri (NDA), fomu itatolewa baada ya kampuni kupokea uthibitisho wa nia ya kushiriki. NDA itaonyesha tarehe ya kutolewa kwa majibu ya maombi.

**Zingatia : Wazabuni waliopita kwenye mchujo tu ndio watakaalikwa kutuma maombi ya zabuni kwa ajili ya mchakato wa zabuni**